

**HISTORIA FUPI YA MAISHA YA  
MAREHEMU FUNDI ANDERSON  
ANDREA MMBANDO LEO TAREHE  
10.11.2022**

**UTANGULIZI:** 2 Wakorintho 13.11 "Hatimaye ndugu, kwaherini; mtimilike, mfarjike, nieni mamoya, mkae katika amani, na Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi"

**KUZALIWA:** Anderson Andrea Mmbando alizaliwa tarehe 15-06-1945 katika kijiji cha Marera Mwika

**KUBATIZWA:** Alibatizwa mwaka 1945 katika Usharika wa Mwika.

**KIPAIMARA:** Alipata mafunzo ya Kipaimara na kubarikiwa tarehe 29-12-1963 katika Usharika wa Mwika.

**ELIMU:** Alipata elimu ya msingi katika shule ya msingi Mwika hadi darasa la 3. Aliendelea na masomo darasa la 4 - 8 Lyakirimu Middle School

- Mwaka 1964 alipata Diploma ya Fundi Radio katika chuo cha The British Tutorial College Arusha
- Mwaka 1971 cheti cha fundi radio toka City and Guilds Of London Institute
- Mwaka 1991 Diploma ya Engineering toka Plymouth College of Further Education , London

**KAZI:** Mwanzoni mwa fani yake ya Uhandisi wa Radio na Umeme, alifanya kazi Tanzania Coffee Board Moshi, Philips Electronics Dar -es- salaam na Philips electronics Nairobi.

**ANDERSON ANDRREA MMBANDO** ni miongoni mwa waanzilishi/mwajiriwa wa mwanzoni wa Redio Sauti ya Injili Moshi (na kabla Manzini Swaziland) kwa takribani miaka 40 mpaka alipostaafu mwaka 2010.

Baada ya kustaafu aliendelea kuwa mshauri (Freelance Consultant) wakujitolea kwa taasisi na mashirika mbalimbali.

**KUOA/UZAO:** **ANDERSON** alimwoa **MAMA EUNICE JOSIA MLAY** tarehe 12-09-1981 katika Usharika wa Mwika. Walijaliwa kupata watoto 4, wakiume 3 na wakike 1

**MARADHI:** **ANDERSON** alikuwa anasumbuliwa na shinikizo la damu, kisukari na kukosa usawa wa kutembea. Alikuwa anapata tiba katika hospitali ya Selian Arusha, Hospital ya Rufaa ya Mkoa ya Mawenzi, Hospitali ya rufaa ya Kanda KCMC na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

**KIFO:** Ilipofika Ijumaa tarehe 04 -11- 2022 saa 4 usiku, nguvu zilimuisha na kuaga dunia akiwa na umri wa miaka 77. Ameacha mjane, watoto 4 na wajukuu 5.

**WASIFU WA ANDERSON MMBANDO**

Alikuwa Mcha Mungu, mcheshi, mshauri mzuri kwa watu wa rika zote. Pia alikuwa mtunza Hazina Mahiri wa

Ukoo na mjumbe wa Halmashauri Kuu ya ukoo toka mwaka 2000 hadi 2010 alipostaafu kutokana na maradhi.

Alikuwa ni fundi wa kweli wa Television, Redio na Antenna za Television. Pia alikuwa mpiga picha maarufu wa kujitegemea. Anderson alikuwa karibu sana na familia yake.

**SHUKRANI:** Familia ya marehemu **ANDERSON** wanapenda kutoa shukrani zao za dhiti kwa ;

1. Mwenyezi Mungu kwa siku alizomjalia ndugu na baba yao hapa duniani
2. Viongozi wa Sharika za Mwika na Karanga mtaa wa Emmanuel kwa huduma zao za Kiroho
3. Jumuiya ya Eden kwa huduma zao
4. Madaktari na wauguzi wa hospital zote alikokuwa anapata tiba.
5. Ndugu na majirani wote waliokuwa wanatoa misaada mbalimbali wakati wa kuuguza
6. Kipekee familia wanapenda kutoa shukrani kwa Mama Martha Eliamani kwa huduma alizotoa tangu mwanzo wa kuuguza hadi mauti yanamfika Baba yetu.
7. Kikundi cha maombi cha MOMS na kikundi cha Kinamama cha Shirimatunda kwa huduma zao za maombi.
8. Ndugu Elihaki Urjo, Peter Kilawe, Freeman Lyimo, Ambrose Kundi na Allen Mlay kwa kuuchukua mwili wa baba yetu usiku na kwenda kuuhifadhi baada ya msiba kutokea

**MWISHO:** 1 Timotheo 4:7 "Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza , imani nimeilinda" . Ameni.